UTT

ni nini?

Gracing Money

Grace Sambali

Finance Systems Writer and
Certified Financial Educator (CFE)

+255 621 685 557

hello@gracingmoney.com

gracingmoney.com

Mwandishi: Grace Sambali

Barua Pepe: hello@gracingmoney.com

Namba ya Simu: 0621 685557

gracingmoney ™

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu yoyote ya kitabu hiki inayoweza kunakiliwa, kutolewa kivuli (photocopy), kuhamishwa, kurekodiwa, kutafsiriwa, au kutolewa kwa namna yeyote bila ya taarifa ya awali ya kimaandishi ya mwandishi.

Kitabu hiki kimeandikwa ili kikupe mwangaza wa kukusaidia kufanya maamuzi chanya ya kukuza uchumi wako. Matokeo ya maamuzi hayo iwe hasi au chanya yatabebwa na wewe, na sio mwandishi wa nakala hii.

Yaliyomo

1. **Maana ya Mfuko wa Pamoja wa Uwekezaji (Mutual Fund...1**
   Kumudu Hatari ya Kupoteza (Risk Appetite)..1

2. **Tofauti Kati ya Mfuko, Hisa, na Hatifungani..2**

3. **Faida za Kuwekeza..3**
   Baadhi ya Mifuko ya Uwekezaji ya Tanzania...5

4. **Maneno Muhimu ya Kufahamu kwenye 'Mutual Funds'..6**

5. **Jinsi ya Kuchagua Mfuko wa Kuwekeza (The Golden Circle)..8**

gracingmoney TM

Yaliyomo

6. Mifuko ya UTT-AMIS……9

Mfuko wa Umoja……10

Mfuko wa Wekeza Maisha……12

Mfuko wa Watoto……14

Mfuko wa Jikimu……16

Mfuko wa Ukwasi (Liquid Fund)……18

Mfuko wa Bond……20

7. Jinsi ya Kupanga Malengo ya Uwekezaji……23

8. Jinsi ya Kuanza Kuwekeza UTT……24

9. Marejeo……26

gracingmoney ™

1. Mfuko wa Pamoja wa Uwekezaji (Mutual Fund)

Ni mfuko ambao watu wengi huwekeza pesa zao na huwa unasimamiwa na wataalamu wa fedha.

Na UTT ni...

Mfuko mama wa pamoja wa uwekezaji, kwetu Tanzania..

gracingmoney™

Kwenye uwekezaji wowote...



...kuna uwezekano wa kupoteza mtaji au fedha.

Wewe kama muwekezaji, unatakiwa kuelewa na kukubali kama unaweza kumudu **kupoteza** fedha **kidogo** (**low-risk** appetite) au anaweza ukamudu **kupoteza zaidi** (**high-risk** appetite).

2. Mfuko wa Pamoja wa Uwekezaji ni tofauti na kuwekeza katika Hisa na Hatifungani

- Mfuko wa Pamoja huwa **unasimamiwa** na wataalamu wa fedha.

- Pesa za kwenye Mfuko huwekezwa katika **rasilimali tofauti** za fedha kama Hisa (Equity/Stocks), Hatifungani (Bonds), Hati za Hazina za Muda Mfupi (Treasury Bills), au Amana za Muda Maalum (Fixed Deposits).

- Mwekezaji wanaweza kuuza vipande vyake vya uwekezaji **kirahisi** (liquidity).

- **Faida** inayopatikana katika uwekezaji **inagawanywa** kwa wawekezaji wote kulingana na idadi ya vipande wanavyomiliki au pesa waliyowekeza.

3. Kwanini unawekeza?

Unapata **faida mbili** ukiwekeza.

Unakuza mtaji wako **(Capital Growth)** au unaongeza kipato **(Income Generation).**

Ukuaji wa Mtaji:

gracingmoney TM

Pesa huendelea kuongezeka au kupungua kulingana na pesa ulioiweka.

Kuzalisha Kipato/Kutoa Gawio:

Mwekezaji anapa kipato katika muda maalumu kulingana na pesa ulioiweka.
Hii inaweza ikawa kila mwezi, kila baada ya miezi mitatu (3), sita (6), au mwaka mmoja (miezi 12).

Gracing Money
UTT AMIS

Kwanini unawekeza?

UTT AMIS ina mifuko sita (6) ya uwekezaji.

Kulingana na malengo yako ya uwekezaji, utachagua mfuko ambao utakuza mtaji au mfuko ambao utakupa kipato. UTT-AMIS ina jumla ya **mifuko sita (6)**.

gracingmoney TM

Kukuza Mtaji

1. Mfuko wa Umoja
2. Mfuko wa Wekeza Maisha
3. Mfuko wa Watoto
4. Mfuko wa Ukwasi

Kupata Kipato/Kutoa Gawio

5. Mfuko wa Jikimu
6. Mfuko wa Bond

Gracing Money
UTT AMIS

Baadhi ya Mifuko mingine ya Pamoja nchini Tanzania...

Ni kama;

- Mfuko wa **Faida** kutoka Watumishi House Investments
- Mfuko wa **Timiza** kutoka Zan Securities
- Mfuko wa **Inuka** kutoka Orbit Securities
- Mifuko ya **iCash, iGrowth, iSave, iIncome,** na **iImaan** kutoka iTrust Finance

gracingmoney TM

4. Kwenye safari yako ya uwekezaji utakutana na maneno kama...

- Thamani Halisi ya Mfuko **(Net Asset Value - NAV)**
  Ni thamani ya mfuko wa uwekezaji baada ya kutoa madeni.

- Thamani Halisi ya Kipande **(NAV per unit)**
  Ni thamani ya kipande kimoja cha mfuko wa uwekezaji. Hii inasaidia kujua bei ya kununua na bei ya kuuza katika mfuko husika.

  Mfano: Kama bei ya kipande kimoja cha mfuko wa uwekezaji ni 100/=, ukulipia 10,000/= ina maana umenunua vipande 100.

- Uwiano wa Gharama (**Expense Ratio**) au Kiwango cha Gharama za Uendeshaji.

  Hii ni asilimia ya mali za mfuko inayotumika kulipia gharama za uendeshaji kama ada za usimamizi, uhasibu, na huduma nyingine za mfuko wa husika.

  Hii gharama huwa ni ndogo na hutegemea pia umewekeza katika mfuko gani.

gracingmoney TM



Mfano:

Mwaka **2005**, Mfuko wa Umoja ulianza na thamani ya kipande **(NAV per unit)** ya 100/= na mfuko ulikuwa na thamani **(Net Asset Value)** ya shilingi Bilioni 108, ila...

Mwaka **2024**, thamani ya kipande ilikuwa imepanda mpaka takribani shilingi 1,050/= na mfuko ulikuwa na thamani ya shilingi Bilioni 360

5. Unachaguaje Mfuko wa Kuwekeza? The Golden Circle

- Je, **kwanini** unataka kuwekeza? Ni **jinsi gani** unataka kuwekeza?, na utawekeza katika **mfuko gani**?

Itabidi utathmini...

Uelewa wako wa Uwekezaji,

Uthubutu wako (**Risk Appetite**),

Mifuko wa Uwekezaji,

Muda wa Uwekezaji,

Namna Utakavyofuatilia (**Investment Tracking**),

Mfuko wako wa Dharura (**Emergency Fund**),

Dhumuni lako la Kuwekeza (**Capital Growth** au **Income Generation**), na

Jinsi ya Kuboresha au Kutoka katika Uwekezaji (**Exit Strategy**)

gracingmoney



Na sasa tuanze...

6. Mifuko ya UTT-AMIS

Mfuko wa Umoja

- Mfuko ulianzishwa mwaka **2005**
- Kwa ajili ya Kukuza Mtaji (**Capital Growth**).
- Malipo baada ya kuuza vipande yanafanyika **ndani ya siku kumi (10) za kazi** baada ya fomu ya mauzo kupokelewa.
- Wanaoruhusiwa kuwekeza na **watu binafsi na taasisi** katika Afrika Mashariki.
- Pesa ya mauzo ya vipande **inakatwa kwa 1.0%** ya thamani ya kipande (NAV)
- Vipande vinaweza kutumika kama **dhamana ya mikopo** kwenye taasisi za fedha
- Hakuna **muda wa kizuizi** cha uwekezaji.
- **Kiasi cha chini** cha uwekezaji ni sawa na thamani ya mauzo ya vipande 10, na
- Hakuna kikomo kwa **kiwango cha juu** cha kuweka.

gracingmoney TM

Mfuko wa Umoja...





SN	Financial Year	Fund Size, Tzs Billion	Performances	
			Returns	Benchmark
01.	2023/24	360.0	12.1%	11.2%
02.	2022/23	320.0	11.2%	7.6%
03.	2021/22	289.0	12.6%	8.7%
04.	2020/21	258.0	16.6%	8.1%
05.	2019/20	226.0	10.3%	1.5%

MGAWANYO

- 60.5% hatifungani na amana za muda mfupi
- 39.5% hisa

Mfuko wa Wekeza Maisha

- Mfuko ulianzishwa mwaka **2007**
- Kwa ajili ya Kukuza Mtaji (**Capital Growth**) kwa muda mrefu (miaka 10)
- Unaruhusiwa kuuza **sehemu ya vipande** baada ya miaka mitano (5)
- Unapata **bima** ya maisha, bima ya ajali na ulemavu wa kudumu, na malipo ya gharama za mazishi
- Anayeruhusiwa kuwekeza ni **Mtanzania (mkazi na asiye mkazi)** mwenye umri wa miaka 18-55
- Pesa ya mauzo ya vipande **inakatwa kwa 2.0%** ya thamani ya kipande (NAV) baada ya miaka mitano (5) ya kizuizi na hakuna makato yoyote baada ya miaka kumi (10)
- Vipande haviwezi kutumika kama **dhamana ya mikopo** kwenye taasisi za fedha
- Mwekezaji anaweza kuchagua:
  (a) Kuwekeza kwa kudunduliza (kiwango cha chini kwa mwezi ni Shilingi 8,340/=)
  (b) Awamu moja (kiwango cha chini ni Shilingi 1,000,000/=)
- Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza na malipo ya bima hayazidi Shilingi TZS 25,000,000/=, na
- Kuna bonasi ya pongezi ya 5% - 7% kama mwekezaji atafikisha miaka 10 ya uwekezaji

gracingmoney
Gracing Money
UTT AMIS

Mfuko wa Wekeza Maisha...





SN	Financial Year	Fund Size, TZS Bn	Performances	
			Returns	Benchmark
1	2023/24	15.2	14.8%	11.2%
2	2022/23	9.2	12.6%	7.6%
3	2021/22	4.4	14.1%	8.7%
4	2020/21	1.8	25.6%	8.1%
5	2019/20	1.4	24.0%	1.5%

MGAWANYO

- 84.5% hatifungani na amana za muda mfupi
- 15.5% hisa

Mfuko wa Watoto

- Mfuko ulianzishwa mwaka **2008**
- Kwa ajili ya Kukuza Mtaji (**Capital Growth**)
- Unaruhusiwa kuuza sehemu ya vipande baada ya mtoto husika kufikisha umri wa **miaka 12**
- Wanaoruhusuwa kuwekeza ni mtu binafsi au taasisi. Mtu huyo awe mtanzania au mwana Afrika Mashariki (mkazi au asiye mkazi). Mtoto anayewekezewa awe na umri chini ya miaka 18.
- Kikomo ni mtoto anapofikisha umri wa **miaka 24**
- Akaunti moja inashikiliwa na mtu mmoja tu
- Pesa ya mauzo ya vipande **inakatwa kwa 1.0%** ya thamani ya kipande (NAV) ndani ya miaka mitatu (3) ya mwanzo na hakuna makato yoyote baada ya miaka mitatu (3)
- Vipande vinaweza kutumika kama **dhamana ya mikopo** kwenye taasisi za fedha
- Utachagua kati ya njia hizi mbili za kuwekeza:
  (a) Scholarship: Kugharamia elimu ya sekondari na kuendelea baada ya umri wa miaka 12, au
  (b) Kukuza Mtaji: hakuna malipo yoyote yatakayofanyika zaidi ya kukuza fedha inayowekezwa
- **Kiasi cha chini** cha uwekezaji ni 10,000/=; Uwekezaji wa ziada wa kila mwezi ni 5,000/=, na
- Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza.

gracingmoney TM

Mfuko wa Watoto…





SN	Financial Year	Fund Size, TZS Bn	Performances	
			Returns	Benchmark
1	2023/24	18.9	14.1%	11.2%
2	2022/23	10.7	12.4%	7.6%
3	2021/22	5.7	14.1%	8.7%
4	2020/21	4.2	19.9%	8.1%
5	2019/20	3.5	12.7%	1.5%

MGAWANYO

- 84.3% hatifungani na amana za muda mfupi
- 15.7% ya hisa

Mfuko wa Jikimu

- Mfuko ulianzishwa mwaka **2008**
- Kwa ajili ya kutoa gawio **kila robo mwaka** au **kila mwaka**. Mtaji hukua kwa kiasi kidogo.
- Malipo baada ya kuuza vipande yanafanyika **ndani ya siku kumi (10) za kazi** baada ya fomu ya mauzo kupokelewa.
- Kwa ajili ya wawekezaji wa Kitanzania (watu binafsi au taasisi)
- Pesa ya mauzo ya vipande inakatwa kwa: 2.0% ya thamani ya kipande (NAV) chini ya mwaka mmoja, 1.5% ndani ya miaka 1-2, 1.0% ndani ya miaka 2-3, na hakuna makato baada ya miaka mitatu (3)
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya kupata mkopo katika taasisi za fedha
- Utachagua kati ya njia hizi za kuwekeza:
  (a) Kukuza mtaji (kiasi cha chini ni shilingi 5,000/=)
  (b) Kupata gawio kila mwaka (kiasi cha chini ni shilingi 1,000,000/=); na
  (c) Kupata gawio kila robo mwaka (kiasi cha chini ni shilingi 2,000,000/=)
- Kiasi cha chini kuongeza hela ni 15,000/= (kwa mpango wa gawio la mwaka na robo mwaka) na 5,000/= kwa ajili ya kukuza mtaji, na
- Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza.

Mfuko wa Jikimu…





SN	Financial Year	Fund Size, TZS BN	Performances	
			Returns	Benchmark
1	2023/24	26.8	13.7%	11.2%
2	2022/23	20.0	13.6%	7.6%
3	2021/22	18.5	13.6%	8.7%
4	2020/21	17.9	18.8%	8.1%
5	2019/20	17.6	15.6%	1.5%

MGAWANYO

- 76.6% hatifungani na amana za muda mfupi
- 23.4% hisa

Mfuko wa Ukwasi (Liquid Fund)

- Mfuko ulianzishwa mwaka **2013**
- Kwa ajili ya **Kukuza Mtaji**
- Malipo baada ya kuuza vipande yanafanyika ndani ya **siku tatu (3)** za kazi baada ya fomu ya mauzo kupokelewa.
- Kwa ajili ya wawekezaji wa Kitanzania (watu binafsi au taasisi)
- **Hakuna makato** unapouza vipande
- Vipande vinaweza kutumika kama **dhamana ya kupata mkopo** katika taasisi za fedha
- Kiasi cha chini cha uwekezaji ni shilingi 100,000/=
- Kiasi cha chini cha ziada ni shilingi 10,000/=, na
- Hakuna kikomo kwa kiwango cha juu cha kuwekeza.

gracingmoney TM

Mfuko wa Ukwasi (Liquid Fund)...





SN	Financial Year	Fund Size, Tzs Bn	Performances	
			Returns	Benchmark
01	2023/24	1,115.0	12.9%	12.3%
02	2022/23	724.7	12.5%	9.7%
03	2021/22	434.7	14.2%	9.3%
04	2020/21	215.9	15.3%	10.1%
05	2019/20	112.8	15.1%	2.3%

MGAWANYO

86.7% hatifungani,

3.9% amana za muda mfupi, na

9.4% amana za muda maalum

gracingmoney

Mfuko wa Bond

- Mfuko ulianzishwa mwaka 2019
- Kwa ajili ya kutoa gawio **kila mwezi** au **kila nusu mwaka**. Mtaji hukua kwa kiasi kidogo.
- Malipo baada ya kuuza vipande yanafanyika **ndani ya siku kumi (10) za kazi** baada ya fomu ya mauzo kupokelewa.
- Unaweza kuuza vipande ulivyonunua miezi sita (6) baada ya kununua (muda wa kizuizi)
- Kwa ajili ya wawekezaji wa Kitanzania (watu binafsi au taasisi)
- Hakuna makato unapouza vipande
- Vipande vinaweza kutumika kama dhamana ya kupata mkopo katika taasisi za fedha
- Utachagua kati ya njia hizi za kuweka:
  (a) Kukuza mtaji (kiasi cha chini ni shilingi 50,000/=)
  (b) Kupata gawio kila mwezi (kiasi cha chini ni shilingi 10,000,000/=); na
  (c) Kupata gawio kila nusu mwaka (kiasi cha chini ni shilingi 5,000,000/=)
- Kiasi cha chini cha ziada ni shilingi 5,000/=, na
- Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza.

gracingmoney

Mfuko wa Bond…





SN	Financial Year	Fund Size, TZS Billion	Performances	
			Returns	Benchmark
01	2023/24	670.3	12.5%	12.3%
02	2022/23	423.6	12.3%	9.7%
03	2021/22	219.8	14.9%	9.3%
04	2020/21	94.5	15.7%	10.1%

MGAWANYO

89.5% hatifungani,

9.7% amana za muda mfupi,

0.8% amana za muda maalum

7. Unapangaje malengo yako ya Uwekezaji?

Vikokotoo | Calculators

- Je, ukiweka kiasi X cha pesa kila mwezi, kitakachorudisha takribani asilimia X% ya faida kwa mwaka, utapata shilingi ngapi baada ya miaka X?

Monthly Investment Calculator
https://uttamis.co.tz/tools/monthly-calculator

- Je, ukiweka kiasi X cha pesa mara moja, kitakachorudisha takribani asilimia X% ya faida kwa mwaka, utapata shilingi ngapi baada ya miaka X?

Single Sum Investment Calculator
https://uttamis.co.tz/tools/single-sum-calculator

gracingmoney™

Unapangaje malengo yako ya Uwekezaji?...

- Je, utaweka shilingi ngapi kila mwezi, kitakachorudisha takribani asilimia X% ya faida kwa mwaka, ili upate kiasi X baada ya miaka X?

  Monthly Investment Plan
  https://uttamis.co.tz/tools/monthly-plan

- Je, utaweka shilingi ngapi mara moja, kitakachorudisha takribani asilimia X% ya faida kwa mwaka, ili upate kiasi X baada ya miaka X?

  Single Sum Investment Plan
  https://uttamis.co.tz/tools/single-sum-plan

gracingmoney™

8. Unaanzaje kuwekeza UTT?

I - Chagua mfuko unaoendana na malengo yako

II - Kufungua Akaunti **kupitia simu ya mkononi**

.Piga ***150*82#** kisha ufuate maelekezo
.Pokea ujumbe na namba ya akaunti yako
.Piga *150*82# tena kisha uweke pin

- Unaweza kuanza kununua vipande papo hapo
- Pia, sio mifuko yote unayoweza kufungua akaunti kwa kupitia simu ya mkononi
- Pakua UTT AMIS kutoka Apple Store au Google Play Store
- Ingia kwenye Mobile App kuangalia akaunti zako
- Tembelea Ofisi za UTT AMIS au Matawi ya Benki ya CRDB kwa Usajili wa Akaunti

Gracing Money UTT AMIS

Unaanzaje kuwekeza UTT?...

III - Kusajili akaunti **kwa kujaza fomu**

Ukiwa na kitambulisho cha taifa, pasipoti,
kitambulisho cha mpiga kura au leseni ya kuendesha gari

Fomu zinapatikana ofisi za UTT AMIS au tovuti (website) ya UTT AMIS.
Ukishajaza, peleka tawi lolote la Benki ya CRDB au uzitume kwa barua pepe (e-mail);
uwekezaji@uttamis.co.tz, operations@uttamis.co.tz, CC marketing@uttamis.co.tz

IV - Akaunti inapofunguliwa, unaweza **kununua vipande** kwa kutumia:

- App ya UTT AMIS
- Mobile Banking kama NMB Mkononi, CRDB SimBanking etc.
- Miamala ya Simu kama M-Pesa, Airtel Money

9. Marejeo:

- https://uttamis.co.tz/
- Annual Report for Invest Life Unit Trust Scheme (Wekeza Maisha Fund) For the Year Ended 30 June 2024
- Annual Report for Umoja Unit Trust Scheme (Umoja Fund) For the Year Ended 30 June 2024
- Annual Report for Children's Career Plan Unit Trust Scheme (Watoto Fund) For the Year Ended 30 June 2024
- Annual Report for Regular Income Unit Trust Scheme (Jikimu Fund) For the Year Ended 30 June 2024
- Annual Report for Liquid Unit Trust Scheme (Liquid Fund) For the Year Ended 30 June 2024
- Annual Report for Hatifungani Trust Scheme (Bond Fund) For the Year Ended 30 June 2024
- https://www.investopedia.com/

gracingmoney